TAARIFA KWA UMMA – AMNESTY INTERNATIONAL

9 Agosti 2023 Nambari ya faharisi: AFR 01/7096/2023

# TAARIFA YA PAMOJA

# MIAKA 20 YA ITIFAKI YA MAPUTO: AZIMIO LISILOFIFIA – KUENDELEZA NA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE NA WASICHANA BARANI AFRIKA

Tunapoadhimisha miaka 20 tangu kuidhinishwa kwa Itifaki ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu kuhusiana na Haki za Wanawake barani Afrika (Itifaki ya Maputo), sisi, mashirika yaliyosaini hapa chini, tunapongeza mafanikio haya ya kuendeleza haki za wanawake na wasichana katika bara hili. Hati hii ya kisheria imeanzisha mfumo kamili unaoainisha viwango ambavyo nchi zinapaswa kuvifuata katika kuendeleza na kulinda haki za wanawake.

Tulitarajia kusherehekea uidhinishaji huu wa Itifaki ya Maputo ulimwenguni kote katika maadhimisho haya adhimu, lakini bado hatujafikia hatua hii muhimu. Idhinisho la Sudani Kusini mnamo Juni 2023 ni jambo la kupongezwa na linatupa matumaini kwamba lengo hili kabambe linaweza kufikiwa. Hii inafanya jumla ya maidhinisho kuwa 44 kati ya 55. Twaziomba Nchi Wanachama zote 11 ambazo bado hazijaidhinisha mkabata huu (Burundi, Botswana, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Misri, Eritrea, Morocco, Madagascar, Niger, Somalia na Sudani) kutimiza ahadi yao ya kutetea haki za wanawake katika nchi zao kwa kuidhinisha na kuchukua hatua zote zinazohitajika ili kuipitisha na kutekeleza Itifaki hii.

## MAENDELEO YALIYOPATIKANA CHINI YA ITIFAKI YA MAPUTO

Katika miongo miwili iliyopita, Itifaki ya Maputo imekuwa na jukumu muhimu katika kuendeleza haki za wanawake na kuwezesha upatikanaji wa haki kutokana na ukiukaji wa haki za binadamu na unyanyasaji. Kwa kutumia Itifaki hii, mahakama za Kenya na Uganda zimetoa maamuzi ya kihistoria yanayothibitisha kukataza ukeketaji wa wanawake (FGM). Tume ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (Tume ya Afrika) iliwawajibisha watendaji kwa kushindwa kuchunguza na kufungua mashtaka ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia dhidi ya wanawake wakati wa maandamano ya vurugu nchini Misri. Katika uamuzi wa kihistoria wa Mei 2018, Mahakama ya Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu ilisema kwamba Mali ilikiuka vifungu kadhaa vya Itifaki hii kuhusiana na umri wa chini wa ndoa, kukomesha aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake, haki ya kuridhia ndoa, haki ya urithi kwa wanawake na watoto waliozaliwa nje ya ndoa, na kukomesha mila na desturi zenye madhara.

Kwa kuzingatia ahadi zilizowekwa katika Itifaki hii, nchi 38 kati ya 55 za Afrika zimetunga sheria na sera zinazolinda haki ya wasichana walio balehe kupata elimu wakati wa ujauzito na uzazi. Niger na Togo ziliondoa sera zinazokataza wanafunzi wajawazito na akina mama vijana kuhudhuria masomo mwaka 2019 na 2022 mtawalia. Uamuzi wa mahakama ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS) ulithibitisha haki ya wasichana wajawazito kupata elimu nchini Sierra Leone na kifungu cha 6 cha Itifaki hii kimetumika kupinga ndoa za kulazimishwa na ndoa za utotoni barani kote.

## UHITAJI WA JUHUDI ENDELEVU KATIKA KUSHUGHULIKIA AINA MBALIMBALI ZA UKATILI WA KIJINSIA

Mafanikio haya pia yanatukumbusha safari ndefu iliyo mbeleni katika kujenga mataifa yenye mshikamano na yaliyo jumuishi ambayo yanaheshimu haki za wanawake. Wanawake wanaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa, ikiwemo ukosefu wa usawa wa kiuchumi, ukosefu wa kufikia ardhi na rasilimali fedha, aina mbalimbali za ukatili wa kijinsia (GBV) na vikwazo katika kupata elimu na huduma za kina za afya, ikiwemo huduma ya afya ya masuala ya ngono na uzazi. Migogoro ya kivita inaendelea kuharibu mfumo wa kijamii wa jumuiya, huku kukiwa na athari kubwa hasa kwa wanawake na wasichana ambao bado wanakabiliwa na unyanyasaji wa kingono na kijinsia kwa kiwango kikubwa kama ilivyokuwa katika migogoro ya Kaskazini mwa Ethiopia na Sudani. Unyanyasaji wa kingono, ndoa za kulazimishwa, ndoa za utotoni, ukeketaji, ukatili, na ubaguzi kwa msingi wa mwelekeo dhahania au halisia wa kingono, utambulisho na udhihirisho wa kijinsia, au sifa za kingono, inasikitisha kwamba bado ni uhalisia ambao wanawake na wasichana wengi wanalazimika kuuvumilia.

Nchi zinapaswa kuweka na kutekeleza mikakati ya kina, ikiwemo mageuzi ya kisheria na mifumo ya uwajibikaji, kampeni za uhamasishaji, elimu ya kina ya masuala ya ngono, ili kuwawezesha watoa huduma za afya kushughulikia mahitaji ya manusura wa

ukatili wa kijinsia. Tunatoa wito kwa nchi wanachama kupitisha kwa haraka mbinu zinazoweka kipaumbele mahitaji na kuzingatia uangalizi wa manusura wa ukatili wa kingono. Mbinu zinazowalenga manusura ni muhimu kwa kuvunja ukimya na unyanyapaa unaozunguka ukatili wa kingono na kuendeleza uponaji, haki, na uwezeshaji wa muda mrefu kwa manusura.

## USAWA WA KIJINSIA UNAHITAJI SERA ZA KIMAGEUZI ZA UCHUMI NA UWEKEZAJI

Licha ya maendeleo makubwa ya haki za wanawake katika miongo miwili iliyopita, kutimizwa kwa haki za kiuchumi za wanawake bado ni mapambano yanayoendelea barani Afrika. Tofauti ya mishahara bado ni tatizo kubwa. Katika nchi za Afrika zilizo chini ya jangwa la Sahara tofauti ya mishahara kati ya wanaume na wanawake inafikia asilimia 30 na ni asilimia 3.9 tu ya wanawake ndiyo wanapata ulinzi wa kijamii. Wanawake wengi wana uwezo mdogo wa kupata mikopo na rasilimali fedha na wanakabiliwa na vikwazo vya kimfumo vya ujasiriamali (ikiwemo kuharamisha sekta isiyo rasmi) na kupata nafasi za uongozi. Aidha, wanawake ndiyo wanaobeba mzigo wa kazi ya ulezi bila malipo, na hivyo kuzuia uwezo wao wa kushiriki kikamilifu katika uchumi rasmi. Ili kufikia usawa wa kweli wa kijinsia, serikali zinapaswa kuchukua hatua madhubuti kuondoa vitendo vya kibaguzi na kuwekeza katika mazingira yatakayowawezesha wanawake kiuchumi. Hii inajumuisha kutekeleza sera zinazohimiza mishahara sawa, kutoa ufikio wa huduma nafuu za ulezi wa watoto, kuhakikisha haki za kumiliki ardhi na mali kwa wanawake, na kukuza mazingira jumuishi ya biashara ambayo yanakubali ujasiriamali wa wanawake ulio rasmi na usio rasmi.

## MIAKA 20 YA ITIFAKI YA MAPUTO: NCHI ZINAPASWA KUONDOA VIKWAZO VYAO NA KUTEKELEZA ITIFAKI ILI KUHAKIKISHA WANANCHI WANANUFAIKA KIKAMILIFU

Suala la baadhi ya nchi kupinga na kuweka vikwazo kwa vifungu muhimu vya Itifaki ya Maputo kuhusiana na haki za afya na uzazi (Ibara ya 14) na ndoa (Ibara ya 6) linaathiri haki za wanawake na wasichana za uhuru wa kimwili na linazuia utekelezaji kamili wa Itifaki. Tume ya Afrika imethibitisha haki za wanawake kudhibiti masuala yanayohusiana na ujinsia wao, ikiwemo, afya ya masuala ya ngono na uzazi, na kuwa huru dhidi ya ulazimishaji, ubaguzi au ukatili katika Maelezo yake ya Jumla Na. 2 kuhusu Ibara ya 14.1 (a), (b), (c) na (f) na Ibara ya 14. 2 (a) na (c). Rwanda na Gambia wameonesha mfano bora kwa kuondoa vikwazo dhidi ya Itifaki hii. Tunatoa wito kwa nchi zote kufanya vivyo hivyo ili kuhakikisha kwamba haki za masuala ya ngono na uzazi na utaratibu wa haki ni mambo yanayofurahiwa na wote.

Katika maadhimisho haya ya miaka 20, tunathibitisha azimio letu thabiti la kushirikiana na Nchi na asasi za kiraia kuendeleza na kulinda haki ya kijinsia barani Afrika. Kupitia utendaji, huruma, na dhamira ya pamoja, tutahakikisha ahadi ya usawa wa kijinsia ni uhalisia halisi kwa kila mwanamke na msichana katika bara hili.

Tunarudia kutoa wito wetu kwa:

- Botswana, Burundi, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Misri, Eritrea, Madagascar, Morocco Niger, Somalia na Sudani kuridhia na kutekeleza kwa haraka Itifaki ya Maputo.

- Cameroon, Ethiopia, Kenya, Mauritius, Namibia, Afrika Kusini na Uganda kuondoa vikwazo vyao vya Itifaki ya Maputo na kuwezesha wananchi wao kunufaika kikamilifu.

- Nchi wanachama wote:
  - Kuwekeza na kuyapa kipaumbele mahitaji ya manusura na hasa manusura wa ukatili wa kingono;
  - Kutekeleza sera zinazohimiza mishahara sawa, ufikio wa huduma nafuu za ulezi wa watoto, haki za kumiliki ardhi na mali kwa wanawake, na mazingra jumuishi ya biashara kwa ajili ya ujasiriamali wa wanawake ulio rasmi na usio rasmi;
  - Kutekeleza sera zinazoimarisha haki ya wanawake kudhibiti masuala yanayohusiana na ujinsia wao na kuhakikisha wote wanafurahia haki za masuala ya ngono na uzazi.

**Watia Saini:**

1. Amnesty International
2. Equality Now
3. FIGO – International Federation of Gynecology and Obstetric
4. SOAWR – Solidarity for African Women's Rights